



HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA OFA YA KUTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA MSIMU WA NANE NANE

Msimu huu wa sikukuu ya Wakulima nanenane, shirika la hifadhi za Taifa-TANAPA linakuletea ofa ewe Mtanzania ya kutembelea hifadhi za Taifa Tarangire, Ruaha na Serengeti.

Huu ni wakati wa kufurahi na familia pamoja na marafiki. Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) linakuhamasisha wewe mtanzania kutembelea hifadhi za Taifa ili ufurahi, ujifunze, uburudike na usefike kwenye mandhari nzuri ya kiasili na kujionea wanyama mbalimbali kama vile twiga, pundamilia, nyumbu, simba, chui, tembo, nyati na wengine wengi wanaopatikana katika hifadhi zetu. Uwapo katika hifadhi zetu, pia utafurahia chakula kizuri na kitamu kwa gharama nafuu kabisa. Wahudumu wetu wenye uzoefu na wakarimu watakuhudumia vizuri

Ili kufanikisha safari hizi TANAPA imeandaa magari maalumu aina ya coater (min bus) yatakayotumika kuwapeleka watalii wa ndani hifadhini.

Ofa hii ni kwa Watanzania tu na zitakuwa kama ifuatavyo:

Safari za kwenda Tarangire na Ruaha zitaanzia jijini Dodoma na zile za kwenda Serengeti zitaanzia mjini Bariadi Mkoa wa Simiyu.

Safari za kwenda Ruaha na Tarangire zitakuwa za kulala na zile za kwenda Serengeti zitakuwa za kutwa (day trip).

Safari zote zitaanza saa 12.00 alfajiri na kurejea jioni siku hiyo kwa safari za kutwa na kesho yake kwa safari za kulala.

Kujiandikisha: Ili kujiandikisha tembelea banda la TANAPA katika viwanja vya nane nane (Nzuguni-Dodoma na Nyakabindi-Simiyu). Ukifika utapewa control

namba utakayotumia kulipia safari hizi. Malipo utayafanya kwa njia ya benki au mitandao ya Simu baada ya kupewa control namba.

VITUO VYA KUONDOKEA:

Dodoma: Magari yataondoka kwenye kituo cha mafuta Puma kilichopo Nyerere square mkabala na CCM Makao Makuu saa 12.00 alfajiri

Simiyu: Magari yataondoka viwanja vya Nyakabindi saa 12.00 alfajiri.

Muhimu:

- Utakapokuja kujiandikisha na kulipia chukua namba ya mhusika wa gari na wewe acha namba yako kwa mawasiliano zaidi.
- Kwa safari za kulala ni muhimu watoto waambatane na wazazi/walezi wao
- Safari za kulala zimezingatia upatikanaji na uwepo wa nafasi ya kulala siku hiyo
- Nafasi ni chache njoo ujiandikishe na kulipia mapema
- Magari yetu yana uwezo wa kubeba watalii 27 tu
- Chakula utajigharamia, bei ya chakula hifadhini ni kuanzia Tsh 7000
- Pesa ikishalipwa haitarudishwa na pia ukichelewa hautarudishiwa
- Mtoto hapa ni yule mwenye umri kuanzia miaka 5 hadi 15

RATIBA YA SAFARI

1. SIMIYU: Safari zitakuwepo kila siku kuanzia tarehe 8/8/2019 hadi tarehe 11/8/2019. Kila siku kutakuwa na gari mbili (2) tu
2. DODOMA KWENDA RUAHA: Safari itakuwepo tarehe 3/8/2019 tu na itakuwa gari moja (1) tu.
3. DODOMA KWENDA TARANGIRE: Safari zitakuwepo tarehe 8/8/2019 gari moja(1) na tarehe 10/8/2019 gari moja(1)

GHARAMA

1. SIMIYU KWENDA SERENGETI: TSH 30,000 WAKUBWA NA TSH 10,000 WATOTO. Gharama hizi zinahusu usafiri, kiingilio, utalii na mwongoza watalii.
2. DODOMA KWENDA RUAHA NA TARANGIRE: TSH 60,000 WAKUBWA NA TSH 40,000 WATOTO. Gharama hizi zinahusu usafiri, kiingilio, utalii, mwongoza wageni na malazi kwenye bandas za TANAPA

Jiachie na jifunze kitalii

KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NASI:-

Email: marketing@tanzaniaparks.com

Simu:

Dodoma: +255 789 831452,0784989572

Simiyu: +255 754089559/0689062291